OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.

SHULE YA SEKONDARI SERENGETI
S.L.P 46,
MUGUMU – SERENGETI.
Simu: +255 743 805 601/+255 786 832 892

Barua pepe: serengetiday.sec@gmail.com

Kumb. Na. SSS/VOL. 1/2022

Mzazi/Mlezi wa ……..

S .L . P ……...

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SERENGETI KIDATO CHA TANO 2022/2023

1.0 Nafurahi kukutaarifu kuwa, mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii ya Sekondari Serengeti kwa mwaka wa masomo 2020/2021, katika tahasusi ya HGL/HKL *(futa isiyohusika)*. Shule ya Sekondari Serengeti ipo umbali wa kilometa04 kusini mwa mji mdogo wa **MUGUMU,** ambao ndio makao makuu ya wilaya ya Serengeti.Usafiri kutoka mjini kuja shuleni unapatikana kwa pikipiki, nauli ni Tsh.2000. Muhula wa masomo utaanza mara tu Serikali itakapotoa tamko mwaka huu.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

a) Sketi mbili (02) za rangi ya kijanijeshi/kombati kitambaa kizito namba moja cha suti zenye marinda ya kawaida kumi na mbili (12) **ndefu sana zinazofunika kifundo cha miguu.**
b) Shati mbili (02) nyeupe zenye mikono mirefu ziwe na mfuko mmoja tu
c) Tai mbili (02) za rangi ya pundamilia (mistari inayokatisha) mieupe na kijani.
d) Fulana/T’ shirt mbili (02) za rangi ya blue nyeusi (dark blue) zenye kola.
e) Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi.
f) Soksi jozi mbili nyeupe nzito zisizo na alama/mistari yoyote.
g) Sweta mbili (02) rangi ya kijani jeshi/kombati kwa ajili ya kujikinga na baridi
h) Nguo za kushindia (shamba dress) gauni mbili (02) kitambaa cha kunguru chenye miraba ya rangi nyeupe na blue bahari (lightblue). Mshono aina ya solo isiyo na marinda yoyote.
i) Track suit moja (01) ya rangi ya dark blue (blue nyeusi)
j) Rangi ya hijab (kijuba) nyeupe isiyokuwa na urembo wowote (kwa waislamu tu)
k) Raba nyeupe za michezo jozi moja. Pamoja na bukta au track suit ya rangi ya blue kwa ajili ya michezo.

Kumbuka: Kama utapata utata/shida katika kutambua rangi za sare ya shule jinsi tulivyoelekeza hapo juu, tafadhali njoo na fedha utapata maelekezo zaidi jinsi ya kuzipata huku **Mugumu.**

3.0 Ada na michango ya shule

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/=. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000/= kwa muhula au kulipa yote. Fedha hizo pamoja na michango mingine ya shule zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na: **30201200053**, Jina la Akaunti ni **SERENGETI SECONDARY SCHOOL RECURRENT A/C NMB.** (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay slip).

b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni kama ifuatavyo:

i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho (fedha hii italipwaa kwenye ofisi ya makamu mkuu wa shule)
iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na Matroni
v. Shilingi 2,000/= nembo ya shule
vi. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza, shule haitahusika na kugharimia matibabu ya mwanafunzi zaidi ya huduma ya kwanza. Tafadhali kila mwanafunzi ajiunge kwenye mifuko ya bima ya afya. (NHIF au CHF).
vii. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya kukodisha godoro kwa muhula, magodoro yanapatikana shuleni (fedha hii italipwa kwenye ofisi ya makamu mkuu wa shule)
viii. Shilingi 5,000/= kwa ajili ya tahadhari (fedha hii haitarejeshwa)
ix. Shilingi 2,000/= kwa ajili ya faili

Kumbuka: Fedha zitalipwa kwenye kupitia akaunti ya shule iliyowekwa hapo juu, isipokuwa ile tu ambayo italipwa ofisi ya makamu mkuu wa shule)

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafuzi anapaswa kuleta/kuja nayo shuleni ni:

i. Ream ya karatasi mbili (02) **A4 aina ya Double A**
ii. Vitabu mbalimbali vya masomo ya tahasusi husika anayokuja kusoma mwanafunzi
iii. Godoro Futi mbili na nusu (75cm) kwa wale ambao wataamua kuja na magodoro yao.
iv. Shuka pair 02, pair moja rangi ya pinki na nyingine rangi ya blue. Blanketi 01, foronya 01 yenye rangi inayofanana na shuka, chandarua kimoja 01 chenye rangi ya blue.
v. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
vi. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko (za plastiki)
vii. Dumu la lita tano (05) kwa ajili ya kuhifadhi maji yake ya kunywa
viii. Ndala au viatu vya wazi kwa ajili ya kuogea na kushindia
ix. Taulo moja (01) kwa ajili matumizi ya mwanafunzi
x. Sanduku la kuhifadhia vifaa vyake (Tunashauri liwe la bati gumu kwa ajili ya usalama zaidi
xi. Jembe 01 lenye mpini wake
xii. Toilet brush moja (01)
xiii. Fyekeo
xiv. Mopper moja (01)
xv. Mfagio mgumu wa kusugulia sakafu (Hard broom)
xvi. Mfagio mlaini (soft broom)
xvii. Mahitaji muhimu mfano Taulo za kike, dawa ya meno, miswaki n.k yasisahaulike
xviii. Madaftari makubwa (Counter books) saba au zaidi
xix. Scientific calculator kwa wanafunzi wa HGL (siyo lazima)
xx. Kalamu za kutosha.
xxi. Kiti na Meza (Au aje na pesa taslimu Tsh. 110,000/=)

MUHIMU: ***NGUO ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIW HIVYO ASIJE NAZO KABISA*.**

4.0 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, walezi na jamii kwa ujumla
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote
vi. Kusuka nywele au kuwa na nywele ndefu shuleni. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote awapo shuleni.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
viii. Uvutaji wa sigara
ix. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuolewa au kuoa
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
xii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule (*Usije na simu)
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

5.0 USAJILI

Mwanafunzi atasajiliwa katika ofisi ya Makamu MKuu wa shule . Hivyo atatakiwa kukabidhi risiti ya malipo pamoja na fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination Form) ambayo itakuwa imejazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. (fomu hii ijazwe kwa usahihi). Vilevile atakabidhi maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki mgomo, fujo na makosa ya jinai. Pamoja na hayo atakabidhi pia Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. Mwisho atakabidhi picha NNE (04) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea shuleni pamoja na namba zao za simu.

(**Picha hizi ziwe za watu ambao majina yao yameandikwa katika fomu maalumu tuliyoambatanisha nyuma)**

Tafadhali , soma kwa makini maelekezo haya na uyatekeleze kwa ukamilifu wake.

“TUNAKUKARIBISHA SHULE YA SEKONDARI SERENGETI”

……..

HAMIS RYOBA MARATATI

MKUU WA SHULE

KUMBUKUMBU MUHIMU ZA MWANAFUNZI

(IJAZWE KABLA YA KURIPOTI SHULENI)

A. JINA LA MWANAFUNZI……..

2.(a)Jina la baba/mlezi ……Passportsize

(b)Kazi ya baba,mlezi……

(c)Mahali anakoishi.

Kijiji/Mtaa……..Kata……..
Wilaya/Mji……Mkoa……

Namba ya simu……Email……

3.(a)Jina la mama/mlezi……Passportsize.

(b)Kazi ya mama,mlezi……

(c)Mahali anakoishi.
Kijiji/Mtaa……..Kata……..
Wilaya/Mji……Mkoa……

Namba ya simu……Email……

B. **NDUGU WA KARIBU.**

NA.	JINA	UHUSIANO	MAHALI NAPOISHI	NAMBA YA SIMU
01				
02				

B. TAMKO LA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO KWA WALIMU NA VIRANJA, UTORO WA VIPINDI/KULALA BWENINI WAKATI WA VIPINDI, MAHUSIANO YA KIMAPENZI, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.

Mimi……..(mwanafunzi), naahidi kuwa

sitajihusisha/sitashiriki katika kupanga, kufanya wala kushabikia migomo kwa walimu na viranja, Utoro wa vipindi na kulala bwenini wakati wa masomo na maandalizi ya usiku (preparation), kuchelewa kuripoti shuleni wakati wa likizo, kutoa lugha chafu kwa walimu, wanafunzi wenzangu, wazazi na watumishi wasio walimu, mahusiano ya kimapenzi, fujo au makosa ya jinai nikiwa Serengeti sekondari katika muda wangu wa uanafunzi.

Sahihi……..tarehe…….

SEHEMU D: TAMKO LA MZAZI/MLEZI

Mimi …….Mzazi/mlezi wa mwanafunzi……..……

Nakiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo ya shule. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi wa shule ya Sekondari ya kutwa Serengeti katika kumlea mwanangu kwenye misingi bora na inayofaa.

Jina la mzazi/mlezi…….....sahihi…….

Tarehe……..Namba ya simu……

SERENGETI SECONDARY SCHOOL

SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

TO THE MEDICAL OFFICER

……..

…….

…….

Name of the Student…….

Form……Term……Year……

Please, kindly examine the above named student to prove his/her fitness undertaking studies at our school.

a) X-ray ( ) 2. Urine ( ) 3. Stool ( )

4. Physical fitness ( ) 5. V.D ( ) 6.Tuberculosis ( )

A: (I) PRELIMINARY INFORMATION (BY THE STUDENT BEFORE THE DOCTOR)

NO	DISEASE	YES/NO	NO	DISEASE	YES/NO
1	Tuberculosis		10	Epilepsy	
2	Pneumonia		11	Ear, Nose and Throat	
3	Asthma		12	Skin disorder disease	
4	Heart trouble		13	Anemia	
5	Recurrent indigestion		14	Operations	
6	Jaundice		15	Serious accident	
7	Kidney and Urinary trouble		16	Malaria	
8	Dysentery		17	Stomach trouble	
9	Nervous breakdown		18	Eye disorder	

(II) VACCINATIONS AND INNOVULATIONS HISTORY

DISEASE	**1ST DATE**	**2ND DATE**	**3RD DATE**
Small pox			
Whoop cough			
Measles			
Yellow fever			
Cholera			

Official

B: MEDICAL EXAMINATION REPORT

a) Weight
b) Heart Beat
c) Vision etc

MEDICAL CERTIFICATE

I have examined the above, and consider that he/she is physically fit/unfit to undergo studies.

DOCTOR'S NAME AND SIGNATURE……...

DATE & OFFICIAL STAMP…….